TOLEO NO.60

# Khilafah

(RAMADHANI 1446 HIJIRIA —MACHI 2025 MILADIA) ( Bei Tsh 2,000/= - Ksh 100/=) NDIO SULUHISHO

## KARIBU RAMADHANI: MWEZI MTUKUFU WA IZZA NA USHINDI




Alhamdullilah, tumeingaia ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, Mwezi wa Rehma, Maghfira, Kuwachwa huru na moto nk. Pongezi kwa Ummah mtukufu wa Kiislamu dunia nzima kwa kuingia katika mwezi wa ibada ya Swaumu. Tunamuomba Allah Taala Atupe tawfiq ya kufunga na kutulipa ujira mkubwa wa mwezi huu.

Ramadhani ni mwezi wa Izzah na ushindi, kwa kuwa ndio ulioteremshwa Quran ambayo ni muongozo thabiti kwa walimwengu wote kwa ajili ya kuwatoa katika viza na kuwapeleka kwenye nuru mpaka siku ya Mwisho. Ndio mwezi aliopewa Utume Mtume wetu (SAAW).

Ramadhani ni mwezi wa izzah na ushindi kwa kutokea matukio makubwa kama ushindi mkubwa katika vita vya Badr,vilivyopiganwa chini ya Mtume SAAW Ramadhani ya pili baada Hijra.
Ni mwezi wa izzah na ushindi kwa kuwa mwaka wa 8 Hijri Waislamu chini ya uongozi wa Mtume (SAAW) walifanya Fathi kubwa ya mji mtukufu wa Makka. Ni mwezi wa Izzah na ushindi kwa kufunguliwa Biladi ya Andalusia (Spain na Portugal) (93 Hijri) chini ya Jemadari Tariq bin Ziyad.
Ni mwezi Izzah kwa Fathi ya mji wa Ommuriyah chini ya Khilafah Al-Mu'tasim (222 Hijri). Ni mwezi wa izza na ushindi kwa vita vya Hittin chini ya Salahuddin Al Ayubi (584 Hijri) kama ilivyo patikana katika vita vya 'Ain Jaloot ndani ya ardhi iliyobarikiwa ya Falastin nk.

Baada ya izza, leo tumo nda ni ya Ramadhani ya 104 tangu kuangushwa Khilafah ya mwisho tarehe 3 Machi 1924 ilhali Umma wetu hauna tena hatamu katika ardhi,na sheria zake hazitekelezwi. Makafiri wametuletea kupitia vibaraka fikra hatari dhidi ya Uislamu wetu kama dini mseto, uzalendo, utaifa, ukabila, haki za wanawake, haki za watoto zinazolenga kuharibu sera za Kiislamu za kijamii na kuichafua jamii ya Kiislamu. Aidha, vibaraka hao huwafungulia milango makafiri kufanya walitakalo katika miji ya Waislamu bila ya kizuizi.
*Inaendelea………….. uk5*

**Yaliyomo**

- *Tahariri uk.2*
- *Kuanguaka Marekani uk 3,*
- *Msikiti uliojengwa na kafiri uk.4*
- *Kuangushwa Khilafah uk.6*
- *Fiqhi ya Ramadhani uk.8*

*RAMADHAN MUBARAK*

## UZINDUZI WA KULIREJESHA TENA JARIDA LA KHILAFAH

Alhamdullilah! tunazindua kulirejesha tena Jarida letu la Khilafah ambalo lilisita kwa muda mwaka 2019 M/1435 H.

Tunalizindua tena ndani ya muda huu wa matukio mawili makubwa:

Tukio la kuanza mwezi mtukufu wa Ramadhani ya mwaka 1446 Hijria.

Tukio la pili ni Kuangushwa dola ya Khilafah ya mwisho (Khilafah Uthmania) na makafiri kwa msaada wa vibaraka katika waturuki na waarabu lililotokea mwezi wa Machi kama huu, mnamo tarehe 03 Machi 1924 M (Rajab 1342 H).

Kurejeshwa jarida la Khilafah katika muda wa matukio hayo mawili sio jambo la sadfa, bali kutokana na uzito na unyeti wa mambo hayo mawili tuliyoyataja

Kuhusiana na tukio la kuanza mwezi wa Ramadhani, hapana shaka fadhila, kheri na utukufu wa mwezi huo ni maarufu, kwetu jarida la Khilafah tunachukua fursa hii ya dhati kutoa mkono wa pongezi kwa Waislamu dunia nzima kwa kuwasili ibada hiyo ya Swaumu.

Pamoja na pongezi hizo pia tunawasisitiza Waislamu kujifunga zaidi na kila ibada na wema ndani ya mwezi huu ili kujikurubisha zaidi kwa Muumba wetu

Amma tukio la kuangushwa Khilafah, hili ni tukio katika matukio makubwa yaliotetemesha Umma mzima. Hili ndio tukio lililokuja kuondoa Maisha ya Kiislamu kwa ukamilifu wake. Bali pia ni tukio lililotua achia majonzi, huzuni na misiba endelevu mpaka leo kwa kuondoshwa ngao ambayo ndio mlinzi wa Waislamu na wanadamu kwa jumla.

Basi ni wajibu kwa Umma mzima wa Kiislamu kufanya kazi usiku na mchana bila ya kuchoka kurejesha tena maisha ya Kiislamu kwa kuirejesha tena ngao hiyo (Khilafah), bali jarida hili la Khilafah limezinduliwa kutoa msukumo wa kulifikia lengo hilo.

Yaani, jarida hili linalenga kuinua ufahamu wa Umma ili ushiriki kikamilifu katika mchakato wa kurejesha tena maisha ya Kiislamu kwa kuirejesha tena dola ya Khilafah iliyoangushwa na makafiri, kwa kuwa jambo hilo ndio ajenda nyeti na kipaumbele cha Umma wa Kiislamu na Uislamu kwa muda huu

Hivyo, ni wazi kwamba kila kitakachochapishwa ndani ya jarida hili iwe katika hukmu, fikra, mitazamo, chambuzi nk. ni kwa mujibu wa mfumo wa Kiislamu tukilenga kuufikisha Umma katika lengo hilo la kurejesha tena maisha ya Kiislamu kwa kupitia kuisimamisha tena dola ya Khilafah inayopaswa kuanzia katika nchi kubwa za Waislamu na kusambaa ulimwenguni kote.

Kwa upande mwingine, lazima tukiri kwamba jarida hili kamwe haliwezi kusonga mbele hata hatua chache bila ya kusomwa, kutolewa mawazo, kuchangamshwa kwa maswali na kusambazwa kwa upana kuwa fikia hadhira ya Waislamu na wanadamu kwa upana.

Ni matumaini yetu kuwa Waislamu na watu jumla watalisoma jarida hili kwa umakini, moyo mkunjufu, mazingatio, na Waislamu kuyabeba kivitendo mafunzo yake kwa kuwa hilo ndio lengo la Uislamu, yaani mafunzo yake yameletwa yaambatane na vitendo na sio nadharia tupu.

Tunawakaribisha wasomaji nyote kwa mikono miwili katika kutupatia mawazo, maoni, rai, maswala nk. ili kufanikisha jarida hili ili liweze kudumu, kuleta matunda na faida kubwa kwa Waislamu na wanadamu kwa jumla. Jopo la waandaaji wa jarida hili wako tayari kupokea changamoto za mawazo, rai na maelekezo ili kulifanikisha

Mwisho, tunakupeni tena mkono wa kheri na kuwatakia Waislamu Ramadhani njema. Uwe mwezi wa neema, barka na nusra kwa Umma wetu mashariki na magharibi. Amiin

Kwa maoni, rai na maswala mbalimbali msisite kuwasiliana nasi .

**Mhariri**

**01Ramadhani 1446 Hijria**

**Machi 2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

# MAREKANI YAANDAMA NJIA YA KUPOROMOKA

Dola yoyote iwe ya kimfumo kama ilivyokuwa Khilafah, Muungano wa Kisovieti, au zilivyo dola za kibepari leo kama Marekani au Uingereza au zisizokuwa za kimfumo kama Himaya ya Roma, Utawala wa Fursi nk hazianguki 'vuu vaa' kama sahani iliyodondoka na kuvunjika. Bali kuanguka kwao huanza kwa viashiria na huwa mchakato wa kidogo kidogo kwa kuandamwa na mapungufu, udhaifu, kupoteza haiba zao hatua baada ya hatua kabla ya kumalizika. Hali hiyo ndivyo inavyodhihirika wazi zaidi kwa dola ya Marekani leo.

Hapana shaka dola za mfumo wa kibepari tangu siku ya mwanzo zimekuwa katika udhaifu na mapungufu kwa kuwa mfumo wao haukujengwa juu ya msingi thabiti na hauwezi kujitetea kihoja, bali wenyewe wamekua mahodari kuweka viraka hapa na pale kuzibaziba madhaifu na mapungufu yao ili walau kurefusha umri wa mfumo huo.

Hata hivyo, kwa kadiri siku zinavyosonga mbele udhaifu wa ubepari na dola zake umekuwa ukidhihirika zaidi na zaidi na kwa muktadha wa dola kama Marekani umekuwa wazi mbele ya macho shahir dhahir.

Kitendo cha dola kubwa kama Marekani kupewa hatamu za uongozi kwa mtu kama Biden aliyekuwa akionekana mara kwa mara kupoteza kumbukumbu zake katika kutaja majina au kuchanganya mambo, hali tunayoweza kukadiria pia kuwepo uwezekano wa Biden kuweza kutoa maamuzi yasio sawa kutokana na kukosa kumbukumbu vyema, ni dalili kwa dola kubwa kama Marekani kuelekea katika mporomoko.

Aidha, kuchaguliwa tena Trump kuwa raisi wa dola hiyo anayeonekana ana vimelea vya umwehumwehu pia si dalili njema kwa kwa nafasi ya dola kama Marekani, na inachora picha ya kuandama njia ya kudondoka. Kwa kuwa dola kubwa hupaswa kuwa na kiongozi makini na mahiri. Alexander the Great aliwahi kusema:

***"Bora kuwa na jeshi la kondoo linaloongozwa na simba, kuliko kuwa na jeshi la simba linaloongozwa na kondoo"***

Kwa upande mwengine, mielekeo, mitazamo ya Trump na baadhi ya hatua na sera zake zinatoa sura ya kudhihirika kudhoofika kwa dola ya Marekani licha ya kuonekana kuwa na maguvu na athari yake kimataifa. Ukiachilia mbali vipaumbele vya Trump kama kupambana na wahamiaji haramu, kuzuiya uraia wa kuzaliwa, jambo linalopingana na katiba yao, pia kuna mambo kadhaa yanayodhihirisha wazi kuifedhehi dola hiyo mchana kweupe, na hatari kwa uhai wa Marekani kwa kupoteza hadhi, haiba na sifa yake kitaifa na kimataifa.

Kauli za Trump za kutaka kulichukuwa eneo la Mfereji wa Panama, eneo la nchi huru inaashiria wazi wazi zaidi mabavu ya Marekani ambayo asili yapo wakati wote, lakini imejifedhehi zaidi. Mfereji huo nyeti sana kwa misafara ya meli na biashara kwa jumla unaounganisha bahari ya Pasifiki na Atlantiki na kupunguza masafa marefu ya usafiri wa meli kwa kuepusha mzunguuko, awali ulianza kujengwa na Ufaransa ndani ya mwaka 1881, kisha Ufaransa ikasita, baadae ujenzi huo ukaendelezwa na Marekani mwaka 1904 na kumalizika 1914. Ujenzi wa mfereji huo ulikuwa na uzito na utata mkubwa wa kiufundi kiasi cha kugharimu maisha ya wafanyakazi wengi. Baada ya kukamilika mfereji huo, kwa makubaliano ukawa unaendeshwa na Panama na Marekani kwa pamoja, ilhali Marekani ikiwa ndio mdau mkuu. Mnamo mwaka 1977 Marekani chini ya raisi Carter na Panama wakafikia mkataba kwamba ifikapo mwaka 1999 mfereji huo ukabidhiwe rasmi kwa nchi ya Panama, na hilo likatekelezwa.

Kauli ya Trump imekumbusha

sura ya tarekhe ya mwelekeo wa kibeberu wa Marekani wa mwaka 1823, mwelekeo unaoitwa 'Monroe Doctrine' ambao ulilifanya eneo la Marekani ya Kusini kana kwamba ni milki ya Marekani

na kuzizuiya kabisa nchi za Ulaya kuingia katika eneo hilo.

Aidha, sera ya utanuzi zaidi ya Trump kimaeneo haikumalizia ndani ya Marekani ya Kusini tu, bali pia alitoa kauli kuhusu kisiwa cha Greenland cha Denmark.

***….Inaendelea.. Uk 7***

# HUKMU YA MSIKITI ULIOJENGWA NA MAKAFIRI

**Swali:**
**Asalaam alaykum** Warahmatullah Wabarakatuh

Nini hukmu ya swala katika msikiti ambao wameujenga makafiri?

**Jawabu:**
Waalaykum Salam Warahmatullah Wabarakatuh

Swali hili lina pande mbili:
Upande wa kwanza: Je inajuzu kuukubali msaada wa kifedha wa kafiri kwa ajili ya msikiti?

Upande wa pili: Je inajuzu swala katika msikiti ambao zimetumiwa kwa ajili yake fedha kutoka kwa makafiri?

Amma upande wa mwanzo, kuhusiana na mchango kutoka kwa makafiri kwa ajili ya msikiti, suala hili lina rai kadhaa… Wako wanavyuoni wanaojuzisha hilo, kwa kutumia qiyasi cha kukubali zawadi kutoka kwa kafiri, na kwamba Mtume (SAAW) alikubali zawadi kutoka kwa Muqauqis ambae ni mtawala wa Misri wa Kiroma… Na ninachokiona mimi kwamba zawadi kwa ajili ya mtu hutofautiana na mchango kwa ajili ya msikiti, uhalisia wake ( waqia) unatofautiana :

1. Hakika ya msikiti ni sehemu ya ibada kwa ajili ya Allah (SWT), kwa hivyo mchango kwa ajili ya msikiti hukubalika (hufahamika) kuwa ni kwa ajili ya Allah (SWT). Na katika Hadithi kutoka kwa Abu Huraira amesema: Kasema Mtume (SAAW :



(مسلم).«أيُّها النّاسُ، إنّ الله طيِّبٌ لا يقْبلُ إلّا طيِّبًا...»

***"Enyi watu hakika Allah ni mzuri hakubali isipokuwa kizuri…" (Muslim).***
Kwa hivyo, haijuzu kukubali mchango kutoka kwa kafiri kwa ajili ya kujenga msikiti kwa sababu mali ya kafiri si nzuri.

2. Na vilevile hakika Mtume (SAAW) ameeleza katika Hadithi zake tukufu kuwa mwenye kujenga msikiti hakika Allah humjengea (mtu huyo) nyumba peponi:
Ametoa Ahmad katika *Musnad* wake kutoka kwa Sa'ad bin Jubair, kutoka kwa Ibn Abas, kutoka kwa Mtume (SAAW) kuwa amesema:
«مَنْ بَنَى لِلَّهِ مَسْجِدًا وَلَوْ كَمَفْحَصِ قَطَاةٍ لِبَيْضِهَا، بَنَى اللَّهُ لَهُ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ».
***"Mwenye kujenga msikiti kwa ajili Allah ijapokuwa kama sehemu anayofukua fukua ndege kwa ajili ya yai lake (yaani msikiti mdogo sana), Allah humjengea msikiti Peponi"***
-Ametoa Tirmidhy katika *Sunan* yake kutoka kwa Uthman bin Affan, amesema: Nimemsikia Mtume (SAAW) anasema:
«مَنْ بَنَى لِلَّهِ مَسْجِدًا بَنَى اللَّهُ لَهُ مِثْلَهُ فِي الْجَنَّةِ»،
***"Mwenye kujenga msikiti kwa ajili ya Allah, atamjengea Allah mfano wake katika Pepo".*** Tirmidhy akasema: Hadithi ya Uthman ni Hadith *Hasan* na *Swahih*.
Na vile vile ameitoa Ibn Khuzaima katika *Swahih* yake kutoka kwa Uthman ibn Affan na ametoa Al-Daramy mfano wake.
-Na ametoa Ibn Hiban katika *Swahih* yake kutoka kwa Abu Dhar amesema: Kasema Mtume (SAAW):
مَنْ بَنَى لِلَّهِ مَسْجِدًا وَلَوْ كَمَفْحَصِ قَطَاةٍ بَنَى اللَّهُ لَهُ بَيْتًا فِي الجنة»
***"Mwenye kujenga msikiti kwa ajili ya Allah ijapokuwa ukubwa wake kama sehemu anayofukua fukua ndege, Allah atamjengea nyumba Peponi". (Sanad* yake ni sahihi).**
Na kwa sababu Hadithi inaonyesha kuwa mwenye kujenga msikiti kwa ajili ya Allah na Allah Taala atamjengea yeye nyumba Peponi, na haliwi hili isipokuwa ni kwa ajili ya Muislamu. Kwahiyo, kilichokusudiwa katika maneno (mwenye kujenga nyumba kwa ajili ya Allah) ni Muislamu huyo, kwa sababu kafiri lau atajenga nyumba hawi katika watu wa Peponi
3. Na vilevile hakika washirikina katika zama za ujinga *(Jahiliyyah)* walijifakharisha kwamba wao ni katika wanaoamirisha Msikiti Mtukufu. Allah akateremsha Aya Tukufu:

﴿أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ وَعِمَارَةَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ كَمَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَجَاهَدَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ﴾

Imeelezwa katika tafsiri ya Qurtubi Kauli yake *Taala:*
﴿أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ...﴾
***"Hivyo mumefanya kuwanywesha maji mahujaji……"***
**Inaendelea uk. 5**

Alama/shaair za Uislamu zinapigwa marufuku. Biladi za Kiislamu zimekatwa vijipande na kukuloniwa na kutawaliwa na vibaraka kwa mkono wa chuma. Makafiri wanaeneza vita kila mahala katika ulimwengu wa Kiislamu ikiwemo ardhi tukufu ya Falastin, kama yanayoendelea Gaza na Ukanda wa Magharibi namna mayahudi wanavyokalia kimabavu ardhi hiyo wakinajisi Masjid Aqswa, kuuwa, kutesa na kudhulumu kiasi cha kuuwa watu 50,000 kuangamiza Gaza yote nk.

Umma unasibiwa na umaskini, unyonge, ujinga, njaa nk. licha ya utajiri wa rasilmali ambazo vibaraka huzivuruga. Kuna vita dhidi yetu vinavyoitwa **Vita vya Ugaidi ambavyo** vimepamba moto kila upande na kuongozwa na Marekani dhidi ya Uislamu na Waislamu

Leo Izzah na ushindi kwa Umma wetu umepotea kwa kuwa Uislamu hautawali katika maisha yetu tangu kuangushwa Khilafah ya mwisho ndani ya mwaka 1924. Katika mwezi huu wa Ramadhani tukumbuke jukumu kuirejesha tena dola ya Kiislamu inayopaswa kuanzia ulimwengu wa Kiislamu. Hiyo ndio dola iliyoutukuza Ramadhani na kuleta Izzah na ushindi.

USIKOSE KUSOMA
JARIDA LA KHILAFAH
KILA MWEZI



Kinachokusudiwa katika lugha ya Kiarabu: Hivyo wamefanya wanaowanywesha maji mahujaji au wenye jukumu la kuwanywesha maji mahujaji ni kama mwenye kuamini Allah na akapigana jihadi katika njia yake.

Na inafaa kukadiriwa kuondolewa (*al-hadhf*) katika maneno ***(Mwenye kuamini),*** yaani "Hivyo mumefanya amali ya kuwanywesha maji mahujaji ni kama amali ya mwenye kuamini".

Na imeelezwa katika tafsiri ya Al-Nasfy: (Hivyo mumefanya kuwanywesha maji mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtukufu ni kama mwenye kumuamini Allah na Siku ya mwisho na akapigana jihadi katika njia ya Allah, hawalingani hawa mbele ya Allah, na Allah hawaongoi watu madhalimu).

Kunywesha maji (assiqaayah) na kuamirisha (al-imarah) ni machimbuko yanayotokana na saqaa na amara ni kama kukinga (aswiyaanah) na ngao (wiqaayah) na hapana budi yenye kutegemea (mudhwaaf) iliyoondolewa ambayo kukadiriwa kwake ni:

﴿أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ وَعِمَارَةَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ كَمَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَجَاهَدَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ﴾

***"Hivyo mumefanya wenye kuwanywesha maji mahujaji na wenye kuamirisha Msikiti Mtukufu ni kama mwenye kumuamini Allah.."***

Na maana yake ni kuwapinga washirikina kuwalinganisha na Waumini na kulinganisha amali zenye kuthibiti na kuwafanya sawa kati yao na kujaalia kuwafanya sawa ni dhulma kwa dhulma yao ya ukafiri, kwasababu wao wameweka kusifiwa na fakhari katika sehemu si zake…)

Na yote haya yanabainisha yule mwenye kukubaliwa kuamirisha Msikiti Mtukufu "na msikiti wowote ule" ni yule mwenye kumuamini Allah na Siku ya mwisho, yaani ni Muislamu. Nalo humaanisha kwa ufahamu wake (*mafhuumih)* ni kutokubali mchango wa kafiri kwa ajili ya kujenga msikiti.

Kwa hivyo, lile ninalolitia nguvu *(urajjihuhu)* ni kutokubali mchango wa makafiri kwa ajili ya kuamirisha misikiti. Na nasema lile ninalolitilia nguvu (*urajjihuhu)* kwa sababu baadhi ya wanavyuoni wanajuzisha mchango kutoka kwa kafiri kama nilivyotaja mwanzo wa jawabu.

Hili ndilo ninalolitilia nguvu.

Na Allah ndie mjuzi zaidi na Mbora zaidi wa hekima.

Haya ni kuhusu upande wa kwanza wa swala.

Ama upande wa pili nao ni kujuzu swala katika hiyo msikiti (lau imetokea kujengwa). Hakika swala inajuzu. Ametoa Bukhari kutoka kwa Jabir bin Abdillah amesema: Kasema Mtume (SAAW):

Mtume (SAAW):

« أُعْطِيتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ مِنَ الأَنْبِيَاءِ قَبْلِي: نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ، وَجُعِلَتْ لِي الأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهُورًا، وَأَيُّمَا رَجُلٍ مِنْ أُمَّتِي أَدْرَكَتْهُ الصَّلاَةُ فَلْيُصَلِّ، وَأُحِلَّتْ لِي الغَنَائِمُ، وَكَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً، وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ كَافَّةً، وَأُعْطِيتُ الشَّفَاعَةَ»

***Inaendelea uk.6***

***"Nimepewa mambo matano ambayo hakupewa Mtume yeyote kabla yangu: Nimenusuriwa dhidi ya hofu kwa mwendo mwezi mzima, na ardhi imefanywa msikiti na safi (yenye kuweza kusafisha) kwa ajili yangu na mtu yeyote katika Umati wangu, ikimdiriki swala basi na aswali, na nimehalalishiwa ngawira, na Mtume (aliyenitangulia kabla yangu) alikuwa anatumwa kwa watu wake maalum,u mimi nimetumwa kwa watu wote, na nimepewa uombezi".***

Na ameitoa Muslim kwa maneno:

Kutoka kwa Jabir bin Abdillah Al-Answary amesema: Kasema Mtume (SAAW):

«أُعْطِيتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ قَبْلِي، كَانَ كُلُّ نَبِيٍّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً، وَبُعِثْتُ إِلَى كُلِّ أَحْمَرَ وَأَسْوَدَ، وَأُحِلَّتْ لِيَ الْغَنَائِمُ، وَلَمْ تُحَلَّ لِأَحَدٍ قَبْلِي، وَجُعِلَتْ لِيَ الْأَرْضُ طَيِّبَةً طَهُورًا وَمَسْجِدًا، فَأَيُّمَا رَجُلٍ أَدْرَكَتْهُ الصَّلَاةُ صَلَّى حَيْثُ كَانَ، وَنُصِرْتُ بِالرُّعْبِ بَيْنَ يَدَيْ مَسِيرَةِ شَهْرٍ، وَأُعْطِيتُ الشَّفَاعَةَ.»

***"Nimepewa mambo matano ambayo hakupewa yeyote kabla yangu, alikuwa kila Mtume anatumwa kwa watu wake maalumu, mimi nimetumwa kwa kila mwekundu na mweusi, na nimehalalishiwa ngawira, hajahalalishiwa yeyote kabla yangu, na ardhi imefanywa kwa ajili yangu kuwa nzuri, safi (yenye kuweza kusafisha) na msikiti, basi yeyote ikimdiriki swala aswali namna alivyo, na nimenusuriwa dhidi ya hofu baina ya mwendo wa mwezi mzima, na nimepewa uombezi"***

Kwa hivyo, sehemu yoyote katika ardhi inajuzu kuswali hapo pindi pakiwa safi (*twaahir)…* kwa hivyo, swala itakuwa ni sahihi katika msikiti wowote hata kama umegharimiwa kifedha na makafiri.

Kutokusihi kukubali fedha kutoka kwa kafiri kwa ajili ya kuamirisha msikiti hakumaanishi kutokubali kuswali humo msikitini. Hayo ni kutokana na tuliyoyabainisha hapo juu.

Haya ndiyo ninayoyatilia nguvu katika mas-ala haya. Allah Taala ndie Mjuzi zaidi na Mbora zaidi wa hekima.

Ndugu yenu Ata bin Khalil Abu Rashta.
Amiri wa Hizb ut Tahrir
27, Muharram 1440H
07, Oktoba 2018

## MATOKEO BAADA YA KUANGUSHWA KHILAFAH

Mwezi kama huu wa Machi tarehe 03 mwaka 1924/ 27 Rajab 1342 H makafiri

wakiongozwa na Uingereza kwa uadui wao na kwa msaada wa vibaraka walifanikiwa kuiangusha Khilafah ya mwisho (Khilafah Uthmania ).

Matokeo ya tukio hilo ni madhila, unyonge, dhulma dhidi ya Umma wa Kiislamu.

Badhi ya yanayotusibu :

1. Umma wa Kiislamu umekosa ibada kubwa, kwani uwepo wa dola ya Khilafah ni ibada katika ibada kubwa.

2. Umma umekosa chombo cha kutekeleza na kusimamia siasa za ndani kama kupitisha hadd, taazir, qisas, uchumi, jamii, elimu nk.

3. Umma umekosa usimamizi wa siasa za nje ambazo zingejenga vyema mahusiano ya Khilafah na dola nyengine na dola hiyo kuwa na sauti na nguvu kimataifa.

4. Umma umekosa kinga ambayo matokeo yake ni uvamizi, mauaji, matesio nk. Mifano hai Afghanistan, Iraq, Gaza, Kashimiri nk.

5. Umma wetu umegaiwa kwa misingi ya matapo na utaifa na kila mmoja akiona hana haja na mwenziwe

6. Umma umetengenezewa na makafiri fikra za maajabu zikanasibishwa na Uislamu kama dini mseto, waswatia nk.

7. Umma na wanadamu kwa jumla wamekosa fursa ya kushuhudia kwa ukamilifu uadilifu na insafu ya Uislamu kivitendo.

Enyi Umma wa Kiislamu

Tukio hili la kuangushwa Khilafah lisimalize kuwa hadithi na huzuni tu kwetu, bali tujifunge na uwajibu wa kuirejesha tena dola hiyo kwa kuanzia katika biladi kubwa za Waislamu, kisha kuenea kila mahala na kuleta ukombozi wa kweli kwa Waislamu na ubinadamu kwa jumla

Kikawaida tumezoeya Marekani kuwa na shauku ya wazi katika ardhi za Waislamu na nchi changa, lakini ujio wa Trump umeonesha hata bara Ulaya hawako salama

Visiwa hivi ambavyo vina kaisi cha mamlaka ya kujiendesha lakini bado ni sehemu ya Denmark viko sehemu nyeti kwa masuala ya kijeshi na usalama, na Marekani kwa muda mrefu hususan baada ya Vita vya Pili imekuwa kimya kimya ina shauku ya kuvitaka, makamo wa raisi wa Marekani Nelson Rockefeller (1974-1977) alifanya jitihada kubwa kisirisiri ya kuvipigania wavipate lakini ilishindikana. Hata hivyo, ujio wa Trump umemfanya kuropokwa wazi shauku yao kwa visiwa hivyo. Jambo lililozuwa taharuki sio tu kwa Denmark bali kwa Ulaya nzima.

Msimamo wa Trump wa kutaka kuwahamisha wakaazi wa Gaza kwa mabavu na kulifanya eneo hilo kuwa ufukwe wa starehe limefemdhehi Trump na pia Marekani, licha ya fedheha kubwa ya kuwa dola hiyo ndiyo iliyokuwa ikitoa msaada mkubwa wa kijeshi ambapo kwa mujibu wa Brown University kuanzia Oktoba 2023 – Oktoba 2024 ulifikia dolari bilioni 17.9:

https://apnews.com/article/israel-hamas-war-us-military-spending-8e6e5033f7a1334bf6e35f86e7040e14

kando na msaada wa kisiasa, kidiplomasia nk. katika kuangamiza maisha ya raia zaidi ya 50,000 wa Gaza na kuuvunja mji wote na kila aina ya miundombinu. Hatua hii ya Trump ni dhidi ya sheria zao wanazoziita za kimataifa, bali ni sehemu ya mauaji ya halaiki. Trump baada ya kauli yake hiyo ya kuipora Gaza na kuwafukuza wakaazi wake kwa nguvu, aliulizwa na mwandishi wa habari wa Marekani. "Unaongelea kuichukua ardhi halali ya watu wenye mamlaka nayo. Unataka kufanya hivyo kwa mamlaka gani ya kisheria? Na jee unazungumzia kuichukua milele, Trump akajibu: "tunataka kuichukuwa na kuwa nayo katika umiliki wetu kwa muda mrefu"

Kitendo cha Trump kuiamrisha Israil hadharani kusitisha mapigano na kuingia makubaliano na Hamas katika masharti ambayo awali Israil iliyapinga sio tu kuifedhehi kambi yao hiyo (Israil) inayolinda maslahi yao ya kimkakati ndani ya Mashariki ya Kati, kimeleta mtifuano kwa baadhi ya wanasiasa wake na kujiuzulu, kinaifedhehi zaidi Marekani yenyewe kwamba ndio mkoloni na muamuzi wa mambo ya Mashariki ya Kati, na kuwafedhehi vibaraka katika ulimwengu wa Kiislamu ambao hufanya kazi ya uwakala wa kuionesha Israili kwamba ni nchi huru inayojitosheleza na ina jeshi kubwa lisiloshindika.

Pia Trump hadharani huwakebehi na kuwadhalilisha vibaraka wa nchi za Kiislamu, kama Misri, Jordan, Saudia nk. Tutakumbuka wakati Trump akisisitiza msimamo wake wa kuhamishwa kwa nguvu Waislamu wa Palestina alisema wazi kwamba Jordan na Misri lazima wawachukue Waislamu wa Palestina, kwa kuwa Marekani imefanya mengi kwa ajili ya dola hizo mbili

Ukiichukua kauli hiyo ya Trump na namna alivyomfedhehi Mfalme wa Jordan mbele yake na ulimwengu katika Ikulu ya Marekani, na alivyojisifu Trump kwa kutangaza hadharani kukwapua mapesa mengi kupitia Bin Salman, mtawala wa Saudia, kwa kumlazimisha kutoa $600 bilioni kuinua uchumi wa Marekani, na Bin Salman akatoa kiasi hicho, na Trump akatamka kwamba atamuamrisha tena mtawala huyo wa Saudia aongeze fedha hizo zifike trillioni nzima. Trump kwa jambo hilo akajisifu hadharani kwamba amediriki kupata fedha hizo kwa kuinua simu moja tu mnamo siku ya 22 Januari 2025. (Al-Hurra America, 23/1/2025)

Fedheha za Trump hadharani kwa watawala wa nchi za Kiislamu ni katika mambo ya hatari kwa mustakabali wa Marekani, kwa kuwa zinasaidia kutoa msukumo wa mabadiliko ya kweli katika ulimwengu wa Kiislamu kwa kuwa Umma unaona wazi wazi kwamba watawala katika nchi zao kumbe ni watumwa tu wa Marekani. Hli hiyo inasaidia kupelekea kuporomoka Marekani. Kwa kuwa vibaraka hao ni katika muhimili nyeti kwa Marekani katika kupora rasilmali, kuulaza Umma na kuzuiya mageuzi ya Kiislamu ya kurejesha tena utawala wa haki wa Khilafah Hayo na mengine mengi ikiwemo namna Marekani ilivyokiuka wazi wazi kanuni zao za kidemokrasia na uhuru wa maoni

*Inaendelea uk 8*

*Kutoka uk.7*

kukabiliana na wimbi la upinzani dhidi ya vita vya aGaza, misimamo na sera nyengine za Trump za kutojali utawala wa sheria, na sera ya kujitenga na washirika wenzake ( wa Ulaya) kiasi cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza John Major 1990-1997 kutamka hadharani kwamba Marekani chini ya Trump inarudi nyuma na kuiacha nafasi yake kama kiongozi wa dunia na inatoa mwanya kwa Urusi na China kupata nguvu zaidi:

https://www.bbc.com/news/articles/c4gwngxdd1vo

Wakati tukiwa katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, mwezi ulioanza chachu ya mabadiliko kwa wanadamu ( kuanza kushushwa Quran) na pia tukiwa katika mwezi huu wa Machi uliotokea tukio kubwa la huzuni la kuangushwa dola ya mwisho ya Kiislamu ya Khilafah Uthmania iliyoangushwa tarehe 3 Machi 1924, na kwa kuzingatia hali ya mdororo wa kuelekea kumalizika dola ya Marekani Umma wetu una wajibu wa kuamka na kubeba jukumu lake la asili la kuurejeshaa ulimwengu utawala wa haki wa Kiislamu kumtawalia mwanadamu na kuongoza wanadamu.



## *YAHUSUYO RAMADHANI*

### MAANA YA SWAUMU

Ni kujizuilia na yale yote yanayofutarisha kuanzia kuingia alfajiri ya kweli mpaka kutua jua (usiku)

### SIFA ZA MFUNGAJI AWE:

Muislamu

Balegh (mtoto anaruhusiwa na inahimizwa kumfundisha kufunga, lakini sio wajibu kwake)

Mwenye akili timamu

Apate taarifa ya kuandama mwezi

### MAMBO YANAYOBATILISHA SWAMU YA RAMADHANI

Kulala usiku wa Ramadhani bila ya nia. Kuweka nia kila usiku (hii ni kwa funga ya Ramadhani tu, amma funga za Sunna inaruhusiwa hata kuweka nia asubuhi)

Kula na kunywa kwa makusudi (itambidi ajizuilie,aombe toba, kisha aje alipe)

Kujitapisha kwa makusudi (itambidi ajizuilie, atubu, kisha aje alipe)

Kufanya jimai (kuingiliana kimapenzi) (itambidi ajizuilie, atubu kisha aje alipe)

Kujitoa manii kwa makusudi (itambidi ajizuilie, atubu kisha aje alipe)

Kupata uwenda wazimu

Kupata heidhi au nifasi kwa mwanamke

Kurtadi (kutoka ndani ya Uislamu)

### MAMBO YANAYODHANIWA KUHARIBU SWAUMU LAKINI HAYAHARIBU

Kula au kunywa kwa kusahau

Kutoka manii kwa bahati mbaya

Kuamka na janaba

Kukoga mchana

Kupaka wanja kwa mwanamke

Kupiga chuku

### WANAORUHUSIWA KULA MCHANA

Wagonjwa wasioweza kufunga

Mama mjamzito

Mama anayenyonyesha

Wasafiri, iwe safari isiyopungua kilomita 81, lakini wakifunga ni bora

Wazee wasioweza kufunga

Wagonjwa wasio na matumaini ya kupoa

### WANAOLIPA FIDIA

Wafuatao wasioweza kufunga watatoa fidia ya kibaba kimoja cha chakula (mchele) kila siku kumpa maskini :

Wagonjwa ambao hakuna tamaa ya kupona

Wazee madhaifu kwa umri mkubwa.

### WENYE WAJIBU WA KULIPA IKIMALIZIKA RAMADHANI

Wagonjwa wa kawaida

Wasafiri

Waliopata heidhi au nifasi

Wote wa kifungu 2 a- e wakiambatanisha na toba.

